

Kumb. No. ISL/VOL.051/2022

30/09/2022

MKURUGENZI WA JIJI  
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA  
S. L. P 1249  
DODOMA

Ndugu, Vincent L. Odera

**YAH: MAREKEBISHO YA GHARAMA ZA KAZI YA ULINZI TULIZOAINISHA KATIKA  
KIDADISI BEI (QUOTATION).**

Husika na mada tajwa hapo juu.

Tafadhali rejea barua yako yenye Kumb. Na; LGA/020/2022-2023/NCS/13- LOT 1 &amp; 3 ya tarehe 30/09/2022.

Tumepokea barua yako ambayo inatuhitaji kujibu kama tumekubaliana na marekebisho ambayo timu yako imeyafanya kama yalivyoainishwa kwenye nukuu ya bei tuliyowasilisha.

1. Nakiri kukosea kwa gharama za kazi ya ulinzi tulizoainisha katika kidadisi bei baada ya timu yangu kuchanganya bei ya katika jedwali kipengele cha Unit Price ambapo hatukujumuisha ongezeko la thamani (VAT) na ongezeko la thamani tulilijumuisha kwenye jedwali la jumla ya gharama kwa mwaka (Amount per Year VAT Inclusive (Tshs)).
2. Hivyo tunakubaliana na marekebisho hayo yaliyofanywa na timu yako kwakuwa marekebisho hayo kweli kimahesabu ni sahihi ila kwa upande wetu yanatubana kwasababu hayana ongezeko la thamani hivyo itatuwia vigumu kulipa mishahara na malipo mengine kulinganana na matakwa ya kisheria kama NSSF, WCF nk.
3. Kilicho tuchanganya timu yangu ni kutoangalia juu ya jedwali ilikuwa imesomeka gharama ikiwa imejumuishwa VAT. Hivyo tunaomba ofisi yako iweze kupokea marekebisho yetu kulingana na matakwa ya zabuni yaliyoainishwa kwenye jedwali la Unit Price yakiwa na ongezeko la thamani ya VAT na Jedwali la jumla ya gharama kwa mwaka haitakuwa na marekebisho yoyote kwa kuwa yapo sawa yamejumuisha ongezeko la thamani VAT.
4. Tutashukuru endapo ombi letu litakubalika na kama gharama yetu ipo ndani ya bajeti yenu na pia endapo tutakidhi vigezo vyote husika ama kama bei ipo chini ya wazabuni wengine walioshiriki tungeomba mtufikirie kupatiwa tuzo ya kutoa huduma ya ulinzi katika Halmashauri yako endapo tutafaulu kwenye kinyang'anyiro.

Tunategemea ushirikiano wako katika shughuli za ujenzi wa Taifa.

Naomba kuwasilisha

INSIGHT SECURITY LTD.

THOMAS STEVEN OSASO  
MKURUGENZI MKUU

